



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Novemba 27, 2022

## **TAARIFA KWA UMMA**

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Eng. Kundo A. Mathew leo Novemba 27, 2022 amefanya ziara ya kikazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na kukagua minara mipya inayojengwa ndani ya Wilaya ya Ludewa ikiwa ni pamoja na mnara unaojengwa na Kampuni Tigo katika Kata ya Lupingu.

Naibu Waziri amepokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ludewa akiwakilishwa na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa Ndg. Daniel Ngalupela, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mbunge wa Jimbo la Ludewa Mhe. Joseph Kamonga, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ludewa pamoja na Wakuu wa Divisheni na Vitengo wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.**